

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129
Nukushi: 026-2322128
Baruapepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



Mji wa Serikali –Mtumba,
Mtaa wa Habari,
S. L. P. 25,
DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

**MWALIKO WA KUTOA MAONI KWENYE MAREKEBISHO YA KANUNI ZA
UTANGAZAJI NA MAUDHUI MTANDAONI**

Dodoma- Agosti 19, 2021

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Innocent Bashungwa, anawakaribisha wadau wa Sekta ya Habari nchini hasa wanaojihusisha na Huduma za Utangazaji na masuala ya utoaji maudhui kwa Umma kupitia mitandao, redio na televisheni kutoa maoni katika Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni za Maudhui Mtandaoni za Mwaka 2020 pamoja na Kanuni za Maudhui ya Utangazaji katika Redio na Televisheni za Mwaka 2018.

Marekebisho haya yamefanywa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 165 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010. Maboresho hayo yatazifanya Kanuni hizo ziendane na maendeleo ya teknolojia pamoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa habari kwa wananchi.

Rasimu za marekebisho ya Kanuni hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara (www.habari.go.tz) pamoja na tovuti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania -TCRA (www.tcra.go.tz).

Maoni yawasilishwe kwa anuani za barua pepe zifuatazo: hglu@habari.go.tz na amina.nguli@habari.go.tz.

Pia, Wizara inawakaribisha wadau wa huduma za utangazaji nchini kufika katika mkutano wa wadau Agosti, 26, 2021, katika Ukumbi wa PSSSF (Zamani - LAMP) Jijini Dodoma, kuanzia Saa 2.00 Asubuhi ili kuhitimisha zoezi la utoaji maoni. Wote mnakaribishwa.

Imetolewa na

John Mapepele

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini